# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU RIPOTI YA SABA YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA ZANZIBAR KWA MWAKA 2022 – 2023.

=====================

**Mheshimiwa Spika;** kila sifa njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma, Muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kufika hapa leo hii tukiwa katika hali ya uzima na amani na kuweza kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika;** pia, nimshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya utulivu, yenye umoja na mshikamano mkubwa, hali ambayo imeendelea kuipa nafasi Serikali na wananchi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na mafanikio mazuri. Aidha, natumia fursa hii kuwasisitiza viongozi na wananchi kwa ujumla kuendelea kuidumisha kikamilifu hali tuliyonayo kwa maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwapa pole wenzetu waliopatwa na maafa ya mafuriko na maporomoko ya udongo katika eneo la Katesh, wilayani Hanang mkoani Manyara ambayo yamepelekea vifo kadhaa na majeruhi, tunamuomba Mwenyezimungu azipumzishe roho za watu hao, na kuwapa subra familia zilizoathirika. Hata hivyo, kamati inampongeza kwa kufupisha safari yake ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi nchini Dubai na


Edit with WPS Office

kurudi nchini kwa ajili ya kushughulikia kwa karibu janga hilo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza na kumshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa utekelezaji bora wa majukumu yake, kujali kwake Utawala wa Sheria na Utawala Bora kwa kuweka mbele matumizi mazuri ya rasilimali kwa faida ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa dhati, kamati inatoa pongezi kwa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora; chini ya Mheshimiwa, Mwl. Haroun Ali Suleiman kwa ufuatiliaji makini wa utendaji katika taasisi anazoziongoza pamoja na mashirikiano anayotupatia. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amzidishie nguvu, afya, hekima na busara katika kazi zake za kumsaidia kiongozi Mkuu wa Nchi. Naomba kukiri mimi pamoja na wajumbe wa kamati hii tumejifunza mambo mengi mazuri katika wizara hii.

**Mheshimiwa Spika;** vile vile, natumia fursa hii kukutakia kheri na siha njema wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili kutoa Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu uwasilishwaji wa Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa Mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa na kwa kuzingatia matakwa ya Wajumbe wa Kamati naomba sasa uniruhusu niwataje Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo: **-**

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Maryam Thani Juma | M/Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Haji Shaaban Waziri | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |
| *8.* | Mhe. Panya Ali Abdalla | Mjumbe |
| *9.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu Msaidizi |


Edit with WPS Office

| | | |
|---|---|---|
| *10.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu Msaidizi |
| *11.* | Ndg. Shawana Mohammed Haji | Katibu Msaidizi |
| *12.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshmiwa Spika;** baada ya utangulizi huo, sasa naomba kutoa maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Ripoti ya Saba ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar ya Mwaka 2022/2023 mbele ya Baraza lako Tukufu kama ifuatavyo: **-**

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inaipongeza Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kutumia vyema Kifungu cha 29 cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Nam. 4 ya 2015 na kuweza kuwasilisha ripoti hii kwa mara ya Saba mfululizo tokea kuanzishwa kwake na kuweza kuonesha mafanikio mbali mbali yaliyofikiwa. Ifahamike kuwa Tume hii imeweka utaratibu wa kuandaa na kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi ya Tume ya Maadili ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya mwaka wa fedha kumalizika kwa Mheshimiwa Rais na kwa maelekezo yake, ripoti hii inatakiwa kuwasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi.

**Mheshimiwa Spika;** kwa ujumla kamati imeridhika kwa kuwasilishwa Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili kwa mwaka 2022/2023 kwa kuzingatia msingi wa kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa kipindi kilichotajwa hapo juu pamoja na ufafanuzi uliotolewa kupitia ripoti hii kwa kuzingatia malengo ya Tume.

**Mheshimiwa Spika;** kamati inasikitishwa na ukiukwaji mkubwa wa maadili kwa kutekeleza majukumu ya umma kinyume na misingi ya maadili ya viongozi ikiwa ni pamoja na matumizi mabaya ya madaraka, matumizi mabaya ya taarifa za Serikali, vitendo vya rushwa mgongano wa maslahi pamoja na matumizi mabaya ya Habari ya teknolojia ya mawasiliano. Kwa msingi huo, kamati inaishauri Tume kuwaasa na kuwachukulia hatua wakuu wa taasisi ambao wanaonesha tabia mbaya katika uongozi wao na kuvunja misingi ya Utawala Bora.


Edit with WPS Office

**Mheshimiwa Spika;** aidha, kamati inaipongeza Tume ya Maadili ya Viongozi kwa kupokea na kusajili taarifa za mali na madeni ya viongozi wa umma zoezi ambalo linaendelea kila siku kwa viongozi wapya pamoja na wale wanaopata uteuzi. Sambamba na hilo, kamati ilitaka kufahamu ni kwa namna gani Tume inawasaidia viongozi wapya walioshindwa kusajili mali zao kutokana na ukosefu wa nyaraka muhimu za uthibitisho wa mali ikiwemo hati za nyumba na mali zisizohamishika. Kamati inaishauri Tume kuwasaidia wateule na viongozi wengine wapya ambao wanataka taarifa za mali zao kwa lengo la kupata hati kwa wakati na kuzitumia kama vielelezo.

**Mheshimiwa Spika;** katika ukusara wa 17 na 18 ambao unaeleza uchambuzi wa malalamiko inaonesha kuwa kosa la matumizi mabaya ya ofisi limechukua nafasi kubwa ukilinganisha na makosa mengine ambayo yamekuwa yakifanywa mara kwa mara katika afisi za umma. Kamati inaishauri Tume kupitia programu zake kuendelea kutoa elimu kwa viongozi ili kuelewa na kufuata masharti ya Sheria na Maadili.  Aidha, kamati inaitaka Tume kuhakikisha viongozi au afisa masuul wa taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali kufuata maadili ya utumishi kwa kutekeleza na kuendesha shughuli za umma kwa kufuata miongozo ya nchi.

**Mheshimiwa Spika;** vile vile, katika uchambuzi wa malalamiko hayo, takwimu zinaonesha kwamba eneo la matumizi mabaya ya madaraka ndio eneo linalolalamikiwa sana na wanajamii huku Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ikiongoza kwa kiasi kikubwa kwa malalamiko hayo. Hivyo, kamati inashauri Serikali kuandaa miongozo na mafunzo au kuzialika taasisi zinazohusika na utoaji wa mafunzo ya maadili na uzalendo kwa viongozi wapya jambo ambalo litawajengea ufanisi katika kada zao. Kwa mnasaba huo, ni muhimu kwa kila kiongozi na kila mtumishi wa umma adhamirie kwa dhati kuongoza na kuongozwa kwa misingi ya uadilifu, uwazi, uwajibikaji na weledi ili juhudi za Serikali ziweze kuzaa matunda katika kujenga utawala bora.

**Mheshimiwa Spika;** kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji


Edit with WPS Office

wa fedha za Matumizi Mengineyo (OC) katika Tume ya Maadili hali inayopelekea kushindwa kukamilisha programu zao mbali mbali wanazojipangia kwa muda unaokusudiwa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya kutosha kwa viongozi na jamii kwa ujumla kutokana na uhaba wa fedha. Aidha, Tume inakabiliwa na uhaba wa vyombo vya usafiri kwa maafisa wake wa Unguja na Pemba, na hivyo, kushindwa kutekeleza vyema majukumu yao ambayo kwa kiasi kikubwa yanahitaji ufuatiliaji. Kupitia hili, kamati inashauri Serikali kuiangalia Tume kwa karibu na kuwapatia vitendea kazi kwa haraka .

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kama tunavyofahamu maendeleo ya nchi yoyote duniani yanategemea na kiwango kikubwa cha uzingatiaji wa maadili katika usimamizi wa rasilimali za nchi ikiwa ni pamoja na utoaji wa huduma bora katika sekta ya umma na binafsi. Aidha, maadili mema yanapaswa kuwa ni sehemu ya mfumo wa jamii. Hivyo basi, tukiwa kama viongozi katika jamii ni wajibu wetu kusimamia vyema ili kudhibiti ukiukwaji wa maadili ya uongozi, mgongano wa maslahi, kujenga taasisi zenye uadilifu pamoja na kutekeleza miongozo ya kisheria ya maadili ya umma.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua hali hii, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua jitihada mbali mbali za kukabiliana na changamoto zinazojitokeza ikiwa ni pamoja na kurekebishwa kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma pamoja na kutoa taratibu na mienendo inayokubalika na isiyokubalika kwa viongozi na jamii nzima. Kwa kutumia nafasi hii kamati inashauri Serikali kuharakisha marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kanuni zake ili kutekeleza majukumu yao kwa kufuata dira na dhamira ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha ripoti hii kwa Wajumbe wa Baraza


Edit with WPS Office

lako Tukufu na ni matarajio yangu tutakuwa kigezo kizuri kwa wananchi na kwa umoja wetu tutaweza kushirikiana kujenga Taifa lenye maadili mema. Sambamba na hilo, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote ambao naiwasilisha hotuba hii. Ni matumaini yangu kuwa ripoti hii itawasaidia viongozi wa umma, wananchi, Taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali katika kusimamia maadili mema na kuimarisha utawala bora nchini.

**Mheshimiwa Spika;** “Naomba Kuwasilisha.”

....................................

(Machano Othman Said)

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

BARAZA LA WAWAKILISHI

<u>ZANZIBAR</u>


Edit with WPS Office